

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 47 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JANUARI 2025

RASIMU YA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WANAIAJIRIWA YAWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama wakifuatilia wasilisho la Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya wanaojiririwa katika utumishi wa umma kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa Tume tarehe 3 Desemba, 2024 mjini Morogoro.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

WALIMU TUTIMIZE WAJIBU TULIOPEWA, SERIKALI NI SIKIVU

Tukiwa tumeuanza mwaka 2025 ni dhahiri kuwa kila Mwalimu amejipanga vizuri kuhakikisha jukumu alilopewa hususan katika kufundisha wanafunzi analitekeleza kwa weledi, bidii na uzalendo ili kuinua sekta ya elimu.

Mwalimu ana wajibu wa kuweka malengo kwa kila somo analofundisha na kuhakikisha anafanya kila linalowezekana ili malengo hayo yaweze kufikiwa huku akitumia zana za kufundishia kwa mujibu wa miongozo ya elimu.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya kazi kubwa katika kuboresha maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kushughulikia


malalamiko yaliyokuwa yanawakabili walimu kwa muda mrefu.

Matarajio ni kwamba katika mwaka 2025, Serikali itaendelea kushughulikia maslahi ya walimu hususan masuala ya upandishwaji vyeo, kulipa malimbikizo ya mishahara, kulipa madai ya fedha za uhamisho na likizo pamoja na kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kufundishia.

Hivyo, kwa upande wa walimu matumaini yetu ni kuwa kila walimu wataongeza juhudi na maarifa katika kutekeleza majukumu yao huku wakizingatia maadili na miiko ya kazi ya ualimu ili kujiepusha na vitendo vya utovu wa nidhamu.

Kheri ya mwaka mpya 2025. Kazi iendelee....

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

RASIMU YA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WANAIAJIRIWA YAWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya akiwasilisha Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya wanaojiririwa katika utumishi wa umma kwenye mkutano wa Tume tarehe 03 Desemba, 2024.

Na mwandishi wetu - Morogoro

Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya wanaojiririwa katika utumishi wa umma iliwasilishwa katika mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 2 Desemba, 2024.

Akiwasilisha rasimu hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu

TSC, Mwl. Fatuma Muya alisema kuwa lengo la wasilisho lilo ni kutoa fursa kwa Makamishna wa Tume kujadili na kupitisha mwongozo huo ili uwasilishwe kenye Mamlaka inayohusika kwa hatua zaidi ikiwa ni sehemu ya utaratibu katika kuandaa nyaraka za namna hiyo.

Mwl. Muya alieleza kuwa Mwongozo huo una lengo la kuwawezesha Walimu kupata uelewa

mzuri wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma kwa ujumla hususani katika Utumishi wa Walimu.

"Vilevile, kupitia mwongozo huu, utasaidia walimu kufahamu haki, wajibu, maadili yanayoongoza Utumishi wa Umma na taaluma ya kada yao kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi ili kuwa na Utumishi wa Umma wenye tija na utoaji wa huduma bora kwa wateja," alisema Mwl. Muya.

Aliongeza kuwa Mwongozo huo utakapokamilika utawapatia walimu wapya taarifa za msingi kuhusu haki na wajibu wao, kuwawezesha kufahamu mbinu bora za kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na kuwasisitiza umuhimu wa kujitambua kama watumishi wanaowajibika kwa jamii na pia kuwapatia maarifa juu ya utunzaji wa kumbukumbu, misingi ya utoaji wa huduma bora kwa wateja, na kuyaelewa mazingira wanayokwenda kufanya kazi.

"Mwongozo huu pia unalenga kuwaelimisha walimu kuhusu taratibu za kupanda madaraja, taratibu na hatua mbalimbali za kinidhamu, na umuhimu wa kudumisha uadilifu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Kwa kutambua mchango wa elimu bora katika maendeleo ya Taifa, Mwongozo huu umeandaliwa kuchochea ari na kujituma kwa walimu wapya ili waweze kushiriki kikamilifu katika kufikia malengo ya kitaifa kwenye sekta ya elimu," alisema Mwl. Muya.


Baada ya wasilisho hilo, Makamishna wa Tume walipata fursa ya kujadili na kutoa maoni katika rasimu hiyo huku wakiipongeza Menejimenti ya TSC kwa kuandaa mwongozo huo ambao utasaidia katika kutoa mafunzo kwa walimu wanaojiririwa katika utumishi wa umma.

RASIMU YA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WANAOGAJIRIWA YAWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Washiriki wa Mkutano wa Tume wakifuatilia wasilisho la Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya wanaogajiriwa katika utumishi wa umma kwenye mkutano wa Tume tarehe 03 Desemba, 2024.

RASIMU YA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WANAOAJIRIWA YAWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU



Washiriki wa Mkutano wa Tume wakifuatilia wasilisho la Rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya wanaojirirwa katika utumishi wa umma kwenye mkutano wa Tume tarehe 03 Desemba, 2024.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

SALAMU ZA POLE

Tume ya Utumishi wa Walimu TSC inatoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki na kwa Watanzania wote kufuatia vifo vya Walimu wanne waliofariki dunia kwa ajali ya gari iliyotokea katika Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.



"Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi amina"



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

SERIKALI YAWAPANDISHA VYEO WALIMU 437 WILAYANI MLELE

**Na Mwandishi wetu –
MLELE.**

Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 imewapandisha vyeo walimu 437 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mlele, Bw. Abel Kundimambwe wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo, 261 ni wa Halmashauri ya Mpimbwe na walimu 176 ni wa Halmashauri ya Mlele.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa jumla ya walimu 16 walibadilishiwa vyeo baada ya kukidhi vigezo ambapo kati yao, walimu

10 ni wa Halmashauri ya Mpimbwe na walimu 6 ni wa Halmashauri ya Mlele.

Bw. Kundimambwe alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2023/24, jumla ya walimu 131 walithibitishwa kazini katika wilaya ya Mlele ambapo Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe walikuwa walimu 66 na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele walikuwa walimu 65.

Bw. Kundimambwe aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutatua kero za walimu na kuhakikisha zimefanyiwa kazi kwa kiwango kikubwa na kuweka mazingira mazuri ya walimu kutekeleza majukumu yao.

Aidha, alisema kuwa Mafunzo yaliyotolewa kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya hivi karibuni yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu.

Aliendelea kueleza kuwa ili kuhakikisha walimu wanazingatia maadili ya kazi yao kushirikisha wadau wengine wa elimu

wamekuwa wakitoa semina na ushauri kwa walimu.

Akizungumzia hali ya mashauri ya nidhamu katika Wilaya ya Mlele, Bw. Kundimambwe

alisema kuwa Mashauri ya nidhamu yaliyowasilishwa yalikuwa tisa (9) ambapo matano (5) yanatoka Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe na mashauri manne (4) yalikuwa yanatoka Halmashauri ya Mlele.

Alisema kuwa kati ya mashauri hayo nane (8) ni ya utoro na shauri moja (1) lilihusu ukaidi na kuongeza kuwa mashauri saba (7) yamefanyiwa uamuzi, wakati mashauri 2 yanasubiri uchunguzi.

Bw. Kundimambwe alisema kuwa katika mashauri saba (7) yaliyofanyiwa uamuzi, walimu watatu (3) walifukuzwa kazi na walimu 4 walipewa adhamu ya onyo.

Wilaya ya Mlele ina jumla ya walimu 1,002 ambapo Mlele ina walimu 382 na Mpimbwe aina walimu 620.

SERIKALI YAENDELEA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU WILAYANI KONDOA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondo, Martin Geoffrey Lugano akitoa mafunzo kwa walimu wakuu hivi katibuni.

Na Mwandishi Wetu-TSC- Kondo

Walimu wilayani k o n d o a w a m e e n d e l e a kutatulia kero m b a m b i l i m b l i zilizokuwa zinawakabili zikiwemo kucheleweshwa kupandishwa vyeo na kubadilishiwa cheo, kutolipwa kwa wakati madi ya fedha za likizo na uhamisho ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mipango ya Serikali ya kuleta mageuzi katika sekta ya elimu na walimu nchini.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 miongoni mwa jitihada zilizofanywa na Serikali katika Wilaya ya Kondo ni pamoja na kuajiri walimu wapya 103 wa Shule za Msingi na 27 wa Sekondari na kupandisha vyeo walimu 891.

Katika idadi ya walimu waliopandishwa vyeo, walimu 578 ni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kondo ambapo Shule za Msingi ni 411 na Sekondari ni 167 na kwa upande wa Halmashauri ya Mji Kondo walimu 313

wamepandishwa ambapo walimu 199 ni wa shule za msingi na 144 ni wa shule za sekondari.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondo, Martin Geoffrey Lugano wakati wa mahojiano na Maaflisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu walipotembelea Ofisi hiyo hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Tume katika kutoa huduma kwa walimu wa Wilaya ya Kondo.

“Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kondo inajivunia sana uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kushughulikia kero na changamoto za walimu,” alisema.

Bw. Lugano aliishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa fedha mbalimbali za kuendeshea Ofisi na kushughulikia masuala ya nidhamu, kuhakikisha walimu wanalipwa haki zao za msingi wanapohitimisha utumishi wao kwa mujibu wa sheria pamoja na kuhakikisha Walimu kupatiwa haki zao za msingi wawapo katika

Utumishi wao kama malipo ya nauli wakati wa likizo, uhamisho na malimbikizo ya mishahara.

“Pia tunashukuru Serikali kwa kutoa mafunzo ya wajumbe wa Kamati ya Wilaya yaliyofanyika mkoani Tabora kwa kanda yetu kwani yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu kwa kuwa na uelewa wa kutosha juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma. Hivyo, imewajengea uwezo mkubwa katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazohitajika,” alisema.

Aliongeza kuwa mafunzo kwa Walimu Wakuu wa Shule yamesaidia kuleta matokeo chanya kwani wamekuwa na uwezo mkubwa wa kutoa elimu kwa walimu wenzao na kushughulikia mashauri mapema kwa kufuata taratibu stahiki kulingana na kanuni na Sheria za Utumishi wa Walimu na kudhibiti masuala ya utovu wa nidhamu kwa walimu.

Bw. Lugano alisema kuwa hatua hiyo imewajengea uwezo na kujiamini katika kuchukua hatua kama mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu.

Alitaja mafanikio mengine ya Serikali kuwa ni kuwezesha walimu kuwa na mazingira rafiki ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu bora ya madarasa, maabara, ofisi, nyumba za walimu na kugawa vishikwambi kwa walimu.

Bw. Lugano alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikishirikiana sana na Ofisi za Wakurugenzi kuhakikisha madeni yanayotokana na likizo na mambo mengine kwa mujibu wa Sheria yalipwa kwa wakati.

Kwa mujibu wa Bw. Lugano, Wilaya ya Kondo ina jumla ya Shule 169 Kati ya shule hizo ambapo Shule za Msingi ni 133 na Sekondari 36 huku ikiwa na walimu 1593 kati ya hao Msingi ni 1071 Sekondari ni walimu 522 ikiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondo ina walimu 1,122 na Kondo Mji ina walimu 471.

SERIKALI YAENDELEA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU WILAYANI KONDOA



Walimu Wakuu wa shule za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wakiwa katika mafunzo yaliyoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondoa hivi karibuni.



Walimu Wakuu wa shule za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wakiwa katika picha ya Pamoja mara baada ya mafunzo yaliyoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondoa hivi karibuni.

TSC NKASI YAMPONGEZA RAIS SAMIA

Na Mwandishi Wetu-TSC-Nkasi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nkasi imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi za kushughulikia kero mbalimbali za walimu ili kuwawekea mazingira mazuri ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Nkasi, Bw. Richard Katyega wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) walipotembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha Uongozi wa Rais Samia.

Alisema kuwa Serikali imefanya kazi kubwa kwa kada ya ualimu kwa kuhakikisha kuwa walimu wanakuwa katika vyeo stahiki na kupewa maslahi bora.

"Ofisi hii inajivunia uongozi wa Awamu ya Sita ilivyoshughulikia kero na changamoto za walimu zikiwemo masuala ya upandishwaji vyeo ambapo walimu waliokuwa wamecheleweshwa kupandishwa vyeo wamepandishwa na wengine kwa mserereko ili kuwa katika vyeo sahihi kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi," alisema.

Alisema kuwa katika kipindi mwaka wa fedha 2023/2024 walimu 771 wamepandishwa vyeo ikiwa walimu wa msingi ni 598 na walimu wa Sekondari 173.

Bw. Katyega alisema kuwa uwepo wa jopo maalum kwa ajili ya uendeshaji wa kliniki ya walimu kumesaidia kutatua kero za walimu wengi kwa wakati mmoja ikiwemo Walimu kupata fursa ya kuzungumza moja kwa moja na Waziri mwenye dhamana ambapo jumla ya walimu 318 wa msingi na sekondari walihudumiwa.

Akizungumzia masuala mengine ya kiutumishi kwa walimu alisema, jumla ya walimu 134 walisajiliwa kwa mwaka 2023/2024, ambapo walimu wa Msingi 81 na walimu wa sekondari 54 na jumla ya walimu 134 wamethibitishwa kazini kwa mwaka 2023/2024, ambapo walimu 81 wa shule za Msingi na walimu 54 wa shule za sekondari.

Aidha, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nkasi Bw. Richard Katyega (kulia) akiwa na Afisa Ajira na Maendeleo Bi. Yusta Luoga wakitekeleza majukumu yao.

Nkasi katika kuhakikisha kuwa usimamizi wa mashauri ya nidhamu yanafanyika kwa ufanisi wameendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya TSC ya Wilaya ili kuwajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Walimu hivyo kuwasaidia kutoa maamuzi sahihi katika vikao vya mashauri ya kinidhamu.

Pamoja na hayo waliendesha Mafunzo kwa Wakuu wa shule ili kuwajengea uelewa kuhusu sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Walimu ambapo inawasaidia kufanya maamuzi sahihi ya kinidhamu kabla ya kufikisha kwa Mwajiri.

Bw. Katyega alisema kuwa pamoja na elimu inayotolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu kutambua umuhimu wa kuzingatia Sheria wakati wa utekelezaji wa majukumu yao bado wapo ambao wanakiuka Sheria na hivyo kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2023/24 Wilaya ya Nkasi ilipokea jumla ya mashauri 16, mashauri 5 ya walimu wa sekondari na 11 ya walimu wa shule za msingi.

Wilaya ya Nkasi ina jumla ya shule za msingi 114 na shule za sekondari 28 ambapo ina jumla ya walimu 1,519 ambapo walimu wa shule za msingi ni 1114 na walimu wa sekondari 405.

TSC, SUMA JKT WAJADILI MIKAKATI YA KUKAMILISHA UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA TUME

Na mwandishi wetu –
Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 2 Desemba, 2024 ilikutana na Mkandarasi, SUMA JKT anayejenga Jengo la TSC Makao Makuu jijini Dodoma kwa ajili ya kupeana mikakati ya kukamilisha mradi huo katika muda wa nyongeza.

Kikao hicho kilichofanyika mjini Morogoro kililenga kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kuboresha utendaji kazi katika mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI ililolitoa tarehe 05 Novemba, 2024.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke na kuhudhuriwa na Makamishna wa TSC na kwa upande wa mkandarasi SUMA JKT uliwakilishwa na Kepteni Emmanuel Mashindi na Mhandisi Elia Ilomo.

Akiwakaribisha wageni hao, Prof. Muruke alisema kuwa Tume inahitaji jengo hilo likamilike kwa haraka ili kuwawezesha watumishi wa Tume hiyo kupata mazingira bora ya kutoa huduma kwa walimu.

Alifafanua kuwa kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi huo na kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI, Tume imelazimika kufanya kikao na mkandarasi huyo ili kuona mpango kazi uliopo kama unaweza kufanya mradi huo kukamilika ndani ya muda



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akiongoza mkutano wa Tume tarehe 2 Desemba, 2024 mjini Morogoro.

wa nyongeza ulioombwa na mkandarasi huyo.

"Tunataka kujua tunakwenda vipi katika kukamilisha mradi huu. Pia ni muhimu sana kuangalia kwa kina mpango kazi uliopo katika kukamilisha mradi huu na kuona kuwa kweli una uhalisia? Mradi utakamilika katika kipindi cha nyongeza kinachooombwa?" akieleza Pro. Muruke.

Akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya ujenzi huo, Mhandisi Ilomo alieleza kuwa hadi kufikia tarehe 2 Desemba, 2024 utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 51.18 na kazi zinazoendelea ni kumwaga zege la sakafu ya tatu (third floor slab), kuweka miundombinu ya umeme

katika sakafu ya chini (ground floor) na sakafu ya kwanza (first floor) pamoja na maandalizi ya kuweka chuma za column za sakafu ya tatu.

"Kazi hizi zina zoendelea sasa za kumwaga zege ya sakafu ya tatu na kuweka miundombinu ya umeme tunatarajia zitakamilika kabla ya tarehe 5 Desemba, 2024 ili tuweze kuanza kazi ya kupiga plasta," alisema.

Katika kikao hicho Mkandarasi, SUMA JKT aliahidi kuwa ili kutimiza malengo ya kukamilisha mradi huo pamoja na kufidia muda uliopotea kutokana na changamoto mbalimbali anakusudia kuongeza muda wa utendaji kazi, kuongeza idadi ya wafanyakazi pamoja na kuongea vitendea kazi.

TSC, SUMA JKT WAJADILI MIKAKATI YA KUKAMILISHA UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA TUME



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo wakati wa Mkutano wa Tume tarehe 2 Desemba, 2024 mjini Morogoro.



Kepteni Emmanuel Mashindi kutoka SUMA JKT akitoa ufafanuzi wa namna ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za Tume Makao Makuu katika mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 2 Desemba 2024 mjini Morogoro.



Mhandisi Elia Ilomo kutoka Mashindi kutoka SUMA JKT akiwasilisha taarifa ya mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za Tume Makao Makuu katika mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 2 Desemba 2024 mjini Morogoro.



Baadhi ya Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakipitia taarifa maendeleo mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu iliyowasilishwa na Mkandarasi wa mradi huo, SUMA JKT katika mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 2 Desemba 2024 mjini Morogoro.



TSC, SUMA JKT WAJADILI MIKAKATI YA KUKAMILISHA UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA TUME



Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika mkutano huo tarehe 2 Desemba 2024 mjini Morogoro.

JITIHADA ZA SERIKALI ZASAIKIA WALIMU WILAYANI KIBONDO WAONGEZA KAZI YA UTENDAJI KAZI

Na Mwandishi wetu – KIBONDO.

"Hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Kibondo zimesaidia walimu kuongeza kazi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao."

Kauli hiyo imetolewa na Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibondo, Bw. Julius Bugagi wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.



Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibondo, Bw. Julius Bugagi akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo ofisini kwakwe hivi karibuni.

Alifafanua kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 imewapandisha vyeo walimu 615 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa 459 na Sekondari walikuwa 156.

Aliongeza kuwa katika mwaka 2023/24 jumla ya walimu 99 walisajiliwa ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 52 na Sekondari 47, walimu 95 walithibishwa kazini na jumla ya walimu 34 waliobadilishiwa vyeo wakiwa wa shule za Msingi 33 na Sekondari mmoja (1).

Alisema kuwa Wilaya ya Kibondo inajivunia uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kupunguza malalamiko ya walimu kuhusu upandishwaji vyeo na kulipa stahiki za walimu.

"Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 615 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu," alisema.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Bugagi alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kibondo imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

Bw. Bugagi alifafanua kuwa jumla ya mashauri ya kinidhamu 19 yalipokelewa ambapo 15 yaliwahusu walimu wa Shule za Msingi na wanne(4) walimu wa shule za Sekondari.

Aliongeza kuwa kati ya walimu hao, tisa (9) walipewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mashahara kwa kipindi cha miaka mitatu, walimu sita (6) walifukuzwa kazi na walimu wanne (4) walikutwa hawana hatia.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kibondo inahudumia jumla ya shule 114 zikiwemo 90 za msingi na 24 za Sekondari huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,166 kwa shule za msingi ni 822 kwa upande wa sekondari ni 322.

SERIKALI YA YATATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU SUMBAWANGA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Sumbawanga, Mwl. Godfrey Michael Kisamo akitekeleza majukumu yake hivi karibuni katika Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sumbawanga.

Na Mwandishi Wetu-TSC- SUMBAWANGA

Tangu Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ilipoingia madarakani mwaka 2021, imefanya kazi kubwa katika kuweka mazingira mazuri katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani Sumbawanga na kutatua kero mbalimbali za walimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi Mwl. Godfrey Michael Kisamo wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu walipotembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha Uongozi wa Rais Samia 2023/24.

Alisema kuwa Serikali imeendelea kutoa fedha kwa Ofisi ya TSC Wilaya

ya Sumbawanga kwa ajili ya kuendeshea vikao vya kisheria na kutatua kero za Walimu hasa katika Upandishwaji Vyeo kwa Walimu kwa msereko na Upandishaji Vyeo ambavyo vilisimama kwa muda mrefu jambo ambalo lilikuwa kama ndoto.

Mwl. Kisamo alisema katika mwakawafedhawa 2023/24, jumla ya Walimu wa Wilaya ya Sumbawanga walipandishwa Vyeo ambapo kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga shule za Msingi walikuwa walimu 889, sekondari 293 na kwa upande wa Manispaa ya Sumbawanga shule ya Msingi walimu 718 na Sekondari 680.

Alisema kuwa katika Wilaya ya Sumbawanga ushughulikiaji wa Madeni ya Walimu umefanyika katika maeneo ya Uhamisho, gharama za masomoni, madai ya malimbikizo ya mishahara, kubadilishiwa vyeo na kupandishwa vyeo kwa msereko kwa watumishi ambao hawapo kwenye vyeo sahihi.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 walimu 109 wamethibitishwa kazini ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Sumbawanga ni 94 na Halmashauri ya Manispaa ni 15 na walimu wapatao watano (05) wamesajiliwa.

Katika hatua nyingine, Mwl. Kisamo alisema kuwa TSC Sumbawanga imekuwa ikikutana na walimu, Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule, Maafisa Elimu Kata na wadau mbalimbali wa Elimu katika kuhakikisha wanawajengea uwezo walimu kuondokana na hali ya kuingia katika Mashauri ya Nidhamu.

Aidha, alisema kuwa wamekuwa wakiwakumbushia walimu kusoma na kupitia Kanuni za Maadili ya Walimu na kupitia vitabu walivyopewa vya "Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi Katika Utumishi wa Walimu: Tume ya Utumishi wa Walimu, 2023"

Mwl. Kisamo alizitaja mbinu wanazotumia kuwasaidia Walimu kukabiliana na changamoto kuwa ni pamoja na kutoa Elimu juu ya kuzingia Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Umma na kuwashauri Waajiri juu ya kuwajibika katika kuwapa Walimu stahiki zao.

Alisema kuwa pamoja na juhudi kubwa zinazotumiwa na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine wapo baadhi ya walimu wanakiuka maadili ya Utumishi wao na kulazimika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ili kuwa fundisho kwa wengine kwa kuzingatia taratibu na Sheria za Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 wameshughulikia mashauri ya kinidhamu matano (5) ikiwa yote ni kutoka shule za msingi yakihusu utoro ambapo walimu wawili (2) wameondolewa katika hatia na mashauri matatu yanaendelea na uchunguzi.

Mwl. Kisamo alisema kuwa Wilaya ya Sumbawanga ina jumla ya Shule 218, kati ya shule hizo, za Msingi ni 177 na Shule za Sekondari ni 41 na kuongeza kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 3,244, kati ya hao, Walimu wa Shule za Msingi ni 2,302 na wa Sekondari ni 942.

SERIKALI YA YATATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU SUMBAWANGA



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Sumbawanga, Bi. Jane Hypolitus Matete akiwa katika Majukumu ya Tume hivi karibuni.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Sumbawanga, Mwl. Godfrey Michael Kisamo (kulia) akiwa kwenye Majukumu ya kazi. Kushoto ni Bi. Sabina Mwajeka(kushoto) akikabidhi taarifa ya kazi.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Sumbawanga wakiwa katika picha ya pamoja.

TSC CHAMWINO YATOA TANO KWA RAIS SAMIA KATIKA UTATUZI WA KERO ZA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu-TSC-
CHAMWINO**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Chamwino imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi za kushughulikia kero mbalimbali za walimu ili kuwawekea mazingira mazuri ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Chamwino, Bi. Paulina Kanumba wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) walipotembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa majukumu ya Tume katika wilaya hiyo.

Bi. Paulina alisema kuwa katika mwaka 2023/2024, Serikali ya Awamu ya Sita imepandisha vyeo Walimu 1,065, walimu 12 wamebadilishwa vyeo na walimu 50 wamepata vyeo vya msrereko wilayani humo.

Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa katika kipindi hicho jumla ya walimu waliosajiliwa na kuthibitishwa kazini walikuwa 130 ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 83 na Shule za Sekondari walikuwa 47.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho walimu wamelipwa na wanaendelea kulipwa madeni yao mbalimbali ambapo walimu wa Shule za Msingi 219 na 290 wa sekondari walipwa madeni ya fedha za likizo na walimu 15 wamelipwa fedha za uhamisho.

Bi. Paulina aliishukuru Serikali

kwa kuwezesha kufanyika kwa Mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Wilaya ambayo yamesaidia kuwaongezea uelewa wa wajibu wao ambao wamesaidia kutoa elimu kwa walimu kwenye shule na maeneo mbalimbali kila wanapopata nafasi.

Aliongeza kuwa Serikali imewezesha kufanyika kwa Mafunzo kwa Wakuu wa Shule ambayo yamesaidia kupunguza mashauri kwani wameelewa wajibu wao na kuchukua hatua kwa ngazi ya shule na kupunguza makosa kwa walimu.

Bi. Paulina alisema kuwa katika kuhakikisha wanasaidia walimu kutoingia katika mashauri ya kinidhamu wamekuwa wakitoa

elimu na ufafanuzi kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Mwalimu.

Alisema kuwa pamoja na jitihada za TSC Wilaya ya Chamwino bado kuna baadhi ya walimu wamekuwa wakijikuta wakikiuka taratibu hizo na hivyo kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kwa mujibu wa Bi. Paulina kwa mwaka 2023/2024 jumla ya walimu 26 walifunguliwa Mashauri ya nidhamu ambayo yalihusu utoro na kughushi ambapo walimu saba (07) walifukuzwa kazi, walimu 19 walipewa adhabu ya kukatwa mshahara asilimia 15 kwa kipindi cha miaka mitatu.

Wilaya ya Chamwino ina jumla ya shule 166 ambapo za Msingi ni 131 na Sekondari ni 35 ambazo zinahudumiwa na TSC huku ikiwa na jumla ya walimu 1,735 ambapo walimu wa shule za Msingi ni 1,195 na Sekondari ni 540.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wa Wilaya ya Chamwino, Bi. Paulina Kanumba akiendelea na majukumu ofisi kwake.

SERIKALI YA YATATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU SUMBAWANGA



Baadhi ya walimu waliotembelea Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu wilaya ya Chamwino hivi karibuni kwa ajili ya kupata ufafanuzi na maelezo mbalimbali yanayohusu haki zao na wajibu.

TSC KONDOA YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WALIMU ILI KUENDELEA KUIMARISHA NIDHAMU KWA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondoa, Geoffrey Lugano akitoa mafunzo kwa walimu wakuu hivi katibuni.

Walimu Wakuu wa shule za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wakiwa katika picha ya Pamoja mara baada ya mafunzo yaliyoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondoa hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu-Kondoa

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kondoa imeendelea na ziara shuleni ili kuwajengea uwezo walimu juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu ili kusaidia walimu kujiepusha na vitendo vya ukiukaji wa maadili ya kazi ya ualimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kondoa, Bw. Geoffrey Lugano wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu walipotembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassani.

Alisema kuwa Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya

Wilaya wamekuwa wakipita shuleni kufafanua kanuni na maadili ya Utumishi wa Walimu kwa walimu na kugawa vipeperushi vyenye miongozo ya kanuni na maadili ya ualimu.

Bw. Lugano aliongeza kuwa wamekuwa wakitoa semina kwa Walimu Wakuu kuhusu Kanuni na Maadili ya Ualimu ili nao watoe elimu hiyo kwa walimu walio chini yao kwa lengo la kuhakikisha kila Mwalimu anatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Alisema kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine ikiwemo Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu na Maafisa Utumishi wamekuwa wakiwajengea walimu uwezo wa kujali kazi na kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma.

Bw. Lugano alisema kuwa pamoja

na juhudi kubwa zinazofanywa na Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kondoa kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine wapo baadhi ya walimu wanaokiuka maadili ya Utumishi wao na hivyo kuilazimu Ofisi ya TSC kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa 2023/2024 wameshughulikia mashauri ya kinidhamu nane (8) ambapo mashauri ya walimu wa shule za msingi yalikuwa matano (5) na Sekondari matatu (3) yote yakihusu utoro.

Bw. Lugano alifafanua kuwa, uamuzi uliotolewa kwa mashauri hayo ni pamoja na kutoa onyo kwa walimu wanne (4), mwalimu mmoja (1) kufukuzwa kazi na walimu watatu (3) kuachiwa huru baada ya kuthibitika kuwa hawana hatia.

TSC BAHİ YAENDELEA KUTOA ELIMU MASHULENI ILI KUIMARISHA NIDHAMU KWA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bahi, Bw. Edward Burton.

Na Mwandishi Wetu-BAHI

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani Bahi kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuwajengea uwezo walimu juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu kwa ajili ya kuwaepusha kujingiza katika vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya kazi ya ualimu na kujikuta wakifunguliwa mashauri ya kinidhamu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bahi, Bw. Edward Burton wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu walipotembelea Ofisi hiyo kwa ajili ya kuapata taarifa ya ya namna Ofisi hiyo inavyotekeleza majukumu yake katika kuhudumia walimu.

Alisema kuwa Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya wamekuwa wakipita katika shule mbalimbali kufafanua kanuni na maadili ya Utumishi wa Walimu kwa walimu

na kugawa vipeperushi vyenye miongozo ya kanuni na maadili ya kazi ya ualimu.

Bw. Burton alisema kuwa ili kupunguza idadi ya mashauri ya nidhamu kwa walimu, TSC Wilaya ya Bahi inatoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya ziara katika shule zote za Msingi na Sekondari, kutoa mafunzo kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa shule na Maafisa Elimu Kata na kusambaza vipeperushi vinavyohusu makosa mbalimbali yanayofanywa na walimu na adhabu zake.

Alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu kutoka Makao Makuu iliendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya ambayo yamesaidia kuleta matokeo chanya kwa Wajumbe kwa kuwapa uelewa mkubwa wa jinsi ya kushughulikia mashauri na kuyatolea uamuzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Bw. Burton aliongeza kuwa katika kuhakikisha walimu wanajengewa uwezo wa kujua Sheria na Kanauni zinazosimamia utumishi wao, Wajumbe wa Kamati za TSC Wilaya nao wamekuwa wakishiriki katika kutoa elimu kwa walimu jinsi ya kuzingatia Kanuni na Taratibu za kazi na kuepuka kufanya makosa ya kinidhamu.

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa mafunzo kwa wakuu wa Shule na Walimu Wakuu yamekuwa yakiwawezesha kutambua kwamba wao ni Mamlaka kamili ya nidhamu kwa walimu katika maeneo yao ya kazi hali iliyosaidia kupunguza idadi ya mashauri ya nidhamu.

Aliongeza kuwa mafunzo kwa Walimu Wakuu wa Shule yamesaidia kuleta matokeo chanya kwani wamekuwa na uwezo mkubwa wa kutoa elimu kwa walimu wenzao na

kushughulikia mashauri mapema kwa kufuata taratibu stahiki kulingana na kanuni na Sheria za Utumishi wa Walimu na kudhibiti masuala ya utovu wa nidhamu kwa walimu.

"Pia tunashukuru Serikali kwa kutoa mafunzo ya wajumbe wa Kamati ya Wilaya yaliyofanyika mkoani Dodoma kwa kanda yetu kwani yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu kwa kuwa na uelewa wa kutosha juu ya Sheria na Kanuni za Ualimu. Hivyo imewajengea uwezo mkubwa katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa walimu na sio utashi binafsi," alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bahi imekuwa ikitoa ushauri nasaha kwa walimu wenye matatizo ya mara kwa mara ya kinidhamu kama njia ya kuwasaidia kujiepusha kutenda makosa.

Bw. Burton alisema kuwa pamoja na juhudi mbalimbali za utoaji elimu kuna baadhi ya walimu ambao wamekuwa wakichukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukiuka Sheria na Kanuni zinazosimamia utumishi wa walimu.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Mashauri ya Nidhamu yaliyopokelewa yalikuwa 17 ambapo mashauri 11 yalitolewa uamuzi, Mashauri mawili (02) yamefanyiwa Uchunguzi na yanasubiri maamuzi ya kikao cha Kamati ya Wilaya na mashauri manne (04) yanaendelea na hatua ya uchunguzi.

Bw. Burton alitaja adhabu zilizotolewa katika mashauri 11 kuwa Walimu nane (08) walipewa

TSC BAHI YAENDELEA KUTOA ELIMU MASHULENI ILI KUIMARISHA NIDHAMU KWA WALIMU

>> INATOKA UK. 20

Karipio, Walimu wawili (02) walifukuzwa kazi na Mwalimu mmoja (1) alishushwa mshahara kwa asimilia 15%.

Alisema kuwa Mashauri yaliyopokelewa na kushughulikiwa yalikusisha makosambalimbali yanayofanywa na walimu kwa kiwango kikubwa ni Utoro kazini, Ulevi, Uzembe wa kutotimiza majukumu na Ukaidi.

Katika hatua nyingine Bw. Burton aliipongeza Serikali ya

Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuendelea kutatua kero na changamoto mbalimbali za walimu zikiwemo za kupanda madaraja/vyeo, kulipa madeni yanayohusiana na mishahara na uhamisho.

“Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bahi inajivunia sana uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kushughulikia kero na changamoto za walimu,” alisema.

Bw. Burton alizitaja changamoto ambazo Serikali imeshughulikia kuwa ni pamoja

na kulipa madeni, kuajiri walimu wapya 101 wa Shule za Msingi 76 wa Sekondari 25 na kuhakikisha walimu wote wenye sifa za kupandishwa vyeo wanapandishwa, na walimu waliojiendeleza kielimu wanabadilishiwa vyeo kwa mujibu wa taratibu.

Alisema kuwa katika kipindi cha Mwaka 2023/2024, TSC Wilaya ya Bahi imesajili walimu wapya 101 na kuwapatia namba za usajili na barua za ajira. Kati ya hao, walimu wa shule za Msingi ni 76 na walimu wa shule za Sekondari ni 25.



Wajumbe wa Kamati ya TSC Wilaya ya Bahi mara baada ya kumalizika kwa kikao cha Pamoja na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu na Maafisa Elimu Kata.



SIKUKUU ZA KITAIFA ZENYE MAPUMZIKO 2025 (NATIONAL PUBLIC HOLIDAYS FOR 2025)

1 Januari (1 st January)	Mwaka Mpya (New Year)
12 Januari (12 th January)	Mapinduzi ya Zanzibar (Zanzibar Revolution Day)
31* Machi au 01* Aprili (31 st * March or 01 st * April)	Eid El- Fitri
7 Aprili (7 th April)	Siku ya kumbukumbu ya Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume (The Sheikh Abeid Amani Karume Day)
18 Aprili (18 th April)	Ijumaa Kuu (Good Friday)
20 Aprili (20 th April)	Jumapili ya Pasaka (Easter Sunday)
21 Aprili (21 st April)	Jumatatu ya Pasaka (Easter Monday)
26 Aprili (26 th April)	Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (Union Celebrations)
1 Mei (1 st May)	Sikukuu ya Wafanyakazi (Workers' Day)
06* au 07* Juni (06 th * or 07 th * June)	Eid El-Hajj
7 Julai (7 th July)	Sabasaba (International Trade Fair)
8 Agosti (8 th August)	Siku ya Wakulima (Peasants Day)
05* au 06* Septemba (05 th or 06 th September)	Maulidi (Maulid Day)
14 Oktoba (14 th October)	Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (The Mwalimu Nyerere Day)
9 Desemba (9 th December)	Uhuru na Jamhuri (Independence and Republic Day)
25 Desemba (25 th December)	Kuzaliwa Kristo (Christmas Day)
26 Desemba (26 th December)	Siku ya Kupeana Zawadi (Boxing Day)

* Sikukuu hizo zinategemea kuandama kwa mwezi. (*Depend on the Sighting of the moon)

Imetayarishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu
(Prepared by Prime Minister's Office)

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kushughulikia stahiki na ustawi wa mwalimu inatakiwa kufuata vigezo, masharti, misingi na taratibu zinazohusu ajira, haki na stahiki za Mwalimu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Utumishi wa Walimu. Stahiki hizo ni pamoja na: -

A. Gharama za Usafiri na Fedha za Kujikimu

Kwa mujibu wa Aya ya 39 ya Kanuni za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2016; Mwalimu anastahili kupatiwa gharama za usafiri na fedha za kujikimu wakati wa: -

- i. Kuajiriwa kwa mara ya kwanza.
- ii. Kuhamishwa kituo cha kazi.
- iii. Usaidizi wa nauli kwenda likizo kulingana na mzunguko husika.
- iv. Kuachishwa kazi.
- v. Kusafiri kwa matibabu.
- vi. Kuhudhuria semina, mikutano na mafunzo kazini.
- vii. Kustaafu.



ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

Gharama za usafiri na kujikimu kwa mwajiriwa wa kwanza, wakati wa mzunguko wa likizo na wakati wa uhamisho zitahusisha mwenza na watoto au wategemezi wanne (4) kulingana na waraka na miongozo ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

B. Gharama za Usumbufu

Kwa mujibu wa Aya ya 41 ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika serikali za mitaa 2016, mwalimu akihamishwa kituo cha kazi na ikamlazimu kuhamisha familia yake, atastahili kulipwa gharama za usumbufu kwa kiwango cha asilimia (10%) cha mshahara wake wa mwaka. Hata hivyo, uhamisho wa kujiombea hautokuwa na malipo ya usumbufu. Mwalimu atakaehama kwa kujiombea na kuruhusiwa na mwajiri, atakuwa na haki na stahiki zote kama mwalimu anayehama katika hali ya kawaida ili mradi mwalimu huyo atakuwa amedumu kwenye kituo hicho cha kazi kwa zaidi ya miaka mitano.

C. Kulipwa Mshahara

Kwa mujibu wa Kanuni ya 20, Kanuni za Utumishi wa Umma 2022, mwalimu ana haki ya kulipwa mshahara kwa viwango vilivyoainishwa na Katibu Mkuu (UTUMISHI) baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma.

D. Kupata fidia kwa magonjwa yanayotokana na kazi au kifo

Aya ya 40 ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu, 2016 inaelekeza, mwalimu atakayepata ugonjwa au kufikwa na umauti katika kutekeleza majukumu ya kazi yake, atafidiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263.

E. Kupandishwa Cheo

Mwalimu akiwa kwenye utumishi wake anastahili kupandishwa cheo kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo vilivyoainishwa chini ya Kanuni ya 8 ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za Mwaka 2016: -

- i. Umahiri, ujuzi na ufanisi wa utendaji kazi wake;
- ii. Kiwango cha elimu alichonacho;
- iii. Sifa binafsi;
- iv. Cheo au orodha ya ukubwa kazini;
- v. Cheo cha mwisho alichonacho;
- vi. Mwajiri kukasimia katika bajeti ya mwaka; na
- vii. Ikama iliyoidhinishwa.

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

Kanuni ya 16, Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022 imesisitiza kuwa mtumishi wa Umma anayepandishwa cheo awekwe kwenye kipindi cha matazamio na anaweza kuthibitishwa ndani ya miezi sita au kuongezewa muda wa matazamio kutokana na uwezo wake kwenye nafasi aliyopewa.

(i) Taratibu za kupandishwa cheo

Upandishaji wa vyeo vya walimu utazingatia masharti ya Kanuni ya 8 ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016: -

- a) Sifa kutokana na kustahili;
- b) Ufanisi na ubora katika utendaji kazi ambao hupimwa kwa (tathmini ya utendaji kazi); na
- c) Ujuzi na sifa binafsi

Utaratibu wa zoezi la kupandisha vyeo walimu kama sehemu ya Watumishi wa Umma linaratibiwa kwa kutegemea Miongozo na Nyaraka zinazotolewa mara kwa mara na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

(ii) Taratibu za kubadilishiwa cheo mwalimu aliyejiendeleza kitaaluma

Mwalimu aliyejiendeleza kitaaluma kutoka ngazi mmoja hadi nyingine atastahili kubadilishiwa cheo kwa kufuata taratibu zifuatazo: -

- a) Mwalimu kuandika barua kwa Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya, kupitia kwa mwajiri wake, kuomba kubadilishwa kazi au kupandishwa cheo akiambatanisha nakala ya cheti husika;
- b) Maombi ya mwalimu husika kuwasilishwa kwenye Kamati ya Tume wa Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya kwa ajili ya kutolewa maamuzi;
- c) Katibu Msaidizi wa Tume wa Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya kumjulisha mwalimu kwa barua kuhusu uamuzi wa Kamati ya Tume wa Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya juu ya ombi lake.

Taratibu za kupandishwa cheo zinaweza kutofautiana kulingana na sifa za mwalimu kama zilivyo ainishwa na/au kwa kutegemeana na maelekezo, miongozo na nyaraka mbali mbali zinazotolewa na serikali.

F. Kupewa Uhamisho

Ili kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji kazi na kutokana na kwa maslahi ya Umma:-

- a) Mwalimu anaweza kuhamishwa kutoka Idara, Wizara, Mkoa au Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda sehemu nyingine (Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016).

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

- b) Mwalimu anaweza kuazimwa kwenye taasisi nyingine ya Umma, binafsi au shirika la Umma kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu. (Aya ya 29 ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2016).

Mwajiri mpya atalipia malipo ya pensheni, marupurupu na kumpa mwalimu husika haki na stahiki zinazoambatana na nafasi hiyo mpya.

G. Kustaafu kwa sababu za kiafya

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022, mwalimu anaruhusiwa kustaafu kwa sababu za kiafya ya mwili au akili ikiwa Mamlaka ya Ajira itajiridhisha kuwa mwalimu husika hawezi kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha au kama mwalimu ataomba mwenyewe. Mamlaka ya Ajira ya mtumishi (mwalimu) inatakiwa kufika kwa daktari aliyeidhinishwa na Mganga Mkuu wa Serikali au Bodi ya Kitabibu iliyoteuliwa na Mganga Mkuu wa Serikali ili kujiridhisha kama mtumishi huyo hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya ugonjwa wa akili au mwili au la. Taarifa ya matokeo ya uchunguzi huo itawasilishwa kwa Mamlaka ya Ajira ambayo ikiridhika, itamstaafisha mtumishi huyo kwa sababu za ugonjwa na kutoa nakala kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI).

H. Kupata Likizo

Mwalimu anastahili kupata likizo mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa Umma. Likizo hizo ni pamoja na-

Aina ya Likizo	Ufafanuzi
i. Likizo ya mwaka	Ni jumla ya siku 28 za likizo kila mwaka ambayo hutolewa kwa mwalimu anayefundisha shuleni muda wa shule kufungwa na kama mwalimu hafundishi shuleni ni kwa kulingana na mzunguko wa likizo yake.
ii. Likizo ya kifo au ugonjwa wa mmoja wa wanafamilia	Ni jumla ya siku 14 kila mwaka ambayo hutolewa kulingana na kifo au ugonjwa wa mmoja wa wanafamilia waliothibitishwa na mwajiri.
iii. Likizo ya uzazi	Ni siku 84 kwa mama aliyejifungua mtoto mmoja na siku 100 kama amejifungua mapacha. Likizo hii ni yenye malipo na hutolewa ndani ya miaka mitatu. Pia mama hupewa ruhusa ya kutoka masaa mawili kabla ya muda wa kazi kuisha kwenda kunyonyesha kwa kipindi cha miezi sita.

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

iv. Likizo ya uzazi kwa baba	Ni siku 5 zinazopaswa kuchukuliwa ndani ya siku 7 kuanzia siku mwenza wake anapojifungua kwa kipindi cha ndani ya miaka mitatu.
v. Likizo ya ugonjwa	Hutolewa kwa malipo kwa miezi sita na kama mwalimu hatopona atapewa tena likizo ya miezi sita kwa malipo ya nusu mshahara. Kama mwalimu hatopona baada ya muda huo, uamuzi wa kumstaafisha kwa sababu za kiafya utafikiriwa.
vi. Likizo bila malipo	Likizo hii inaweza kuombwa na kutolewa na Katibu Mkuu anayejihusisha na UTUMISHI akiridhika kuwa ina manufaa kwa Umma. Maombi yake yatafanyika kupitia Mwajiri ambaye atawasilisha kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI). Likizo hii inaweza kuombwa ikiwa mwalimu anataka kushiriki nafasi za uongozi wa kisiasa, kufanya kazi kwenye mashirika ya kikanda au kimataifa.
vii. Likizo ya kabla ya kustaafu	Huchukuliwa mwezi mmoja kabla ya tarehe ya kustaafu.
viii. Likizo ya kujiendeleza Kitaaluma au kiutaalamu	Ni kipindi cha miezi 12 ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Maombi ya likizo ya kujiendeleza kitaaluma au kielimu na likizo bila malipo hufanywa na mtumishi husika yakielekezwa kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) na maombi husika sharti yapitie kwa Mwajiri.

I. Huduma ya Afya

Kila mwalimu anastahili kupata huduma ya afya kwake, mwenza na watoto au wategemezi wasiozidi wanne (4) isipokuwa tu kama sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa zimeweka vigezo tofauti. Pia, mwalimu anayo haki ya kulindwa dhidi ya afya yake wakati wa kutekeleza majukumu yake.

J. Kustaafu

Mwalimu anaruhusiwa kustaafu kwa hiari au kwa lazima.

- a) **Kustaafu kwa hiari:** Hii ni pale mwalimu anaomba mwenyewe kustaafu akifikia umri wa miaka 55.

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

b) Kustaafu kwa lazima: Hii ni pale mwalimu anastaafu akifikisha umri wa miaka 60.

Aidha, kwa marekebisho ya Kanuni 47 ya Kanuni za Kudumu za 2009, inapotokea mgogoro wa tarehe ya kuzaliwa baina ya nyaraka moja na nyingine za mtumishi husika, nyaraka yenye kuonesha umri mkubwa ndiyo itatumika kuwa ndiyo tarehe sahihi ya kuzaliwa mtumishi huyo.

Mambo muhimu mwalimu anatakiwa kuzingatia wakati wa kustaafu ni pamoja na:-

- i. Kuwasilisha katika ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya, barua iliyoambatanishwa na nyaraka inayoonesha umri wa mwalimu.
- ii. Tume kufanyia kazi kwa kuhakiki barua na nyaraka zilizowasilishwa kwake ,pamoja na nyaraka zilizoko kwenye jalada la mwalimu; na
- iii. Tume kutoa kibali cha kustaafu baada ya kujiridhisha na taarifa za mwalimu.

Ni jukumu la Mwajiri kuandaa taarifa za kiutumishi za mwalimu na kuziwasilisha kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii ambapo mtumishi alikuwa anachangia. Ukokotoaji na Ulipaji wa mafao ya hifadhi ya jamii hulipwa na mifuko ya hifadhi ya jamii.

K. Kuacha Kazi

Aya ya 60 ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2016, mwalimu anaweza kuacha kazi kwa kumpa mwajiri wake notisi ya miezi mitatu (3) au mshahara wa mwezi mmoja (1) badala ya notisi. Mwalimu mwenye mkataba wa kuendelea kumtumikia mwajiri baada ya kumaliza masomo anatakiwa atimize masharti ya Mkataba (bondi) na amalize madeni yake kwa mwajiri kabla ya kuomba kuacha kazi.

L. Kupewa Cheti cha Utumishi

Aya ya 61 ya Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2016 imeeleza kuwa, ikiwa ajira ya mwalimu imesitishwa au amestaafu katika nafasi yake ya utumishi, mwajiri wake anatakiwa kumpa cheti cha utumishi.

M. Gharama za Mazishi

Mwalimu akifariki akiwa kazini, au akifiwa na mwenza au mtoto anayetambulika, mwajiri wake atagharamia vitu vifuatavyo:-

- i. Jeneza;
- ii. Kaburi/kuchimba kaburi;
- iii. Sanda;
- iv. Shada la maua; na

ZIFAHAMU STAHIKI ZA MWALIMU

- v. Usafiri wa kusafirisha mwili mpaka sehemu anapoishi, au sehemu yoyote itakayokuwa imeamriwa na ndugu wa marehemu kwa ajili ya mazishi.

Mwalimu ataruhusiwa kuhudhuria mazishi ya ndugu wa karibu (baba, mama, mwenza na watoto kwa muda usiozidi siku kumi na nne (14). Likizo hii itakuwa ya malipo ya mshahara na haitakatwa kwenye likizo ya mwaka. Likizo hii haitakuwa na malipo ya usafiri, marupurupu au posho. (Kanuni 62, Kanuni za Serikali za Mitaa, Mwenendo wa Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu, 2016)

N. Kupata taarifa

Aya za 23 (3) na (25) za Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2016 imebainisha kuwa, mwalimu ana haki ya kupata taarifa sahihi anazozihitaji kuhusu utumishi wake. Mwajiri au msimamizi atahakikisha mwalimu anapata taarifa na nyaraka na vitendea kazi vyote. Mwalimu atahakikisha anakuwa na hizo nyaraka, anazielewa, kuzitumia na kupata tafsiri sahihi za sheria na nyaraka alizopewa.





SALAMU ZA MWAKA MPYA ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, KWA WATANZANIA, TAREHE 31 DISEMBA, 2024

SALAMU ZA MWAKA MPYA ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, KWA WATANZANIA, TAREHE 31 DISEMBA, 2024

Ndugu Wananchi;

Leo, tarehe 31 Disemba, tunauhitimisha mwaka 2024 na kuukaribisha mwaka 2025. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa neema ya uhai na afya njema. Wapo wenzetu wenye changamoto za kiafya, ambao tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema ili warudi kwenye shughuli zao za kujenga Taifa.

Kuna ndugu na jamaa zetu ambao tungetamani kuwa nao leo hii, lakini kwa mapenzi yake Mola, haikuwezekana. Tuendeleo kuwaombea mapumziko mema peponi. Amen

Ndugu Wananchi;

Mwaka 2024 ulikuwa mwaka wa kihistoria, wenye mafanikio na unaotupa matumaini zaidi tunapoitazama kesho ya Taifa letu. Katika jitihada za kutekeleza majukumu yangu, nilipata fursa ya kufanya ziara katika baadhi ya Mikoa, na kote nilikopita nimejionea ari na hamasa kubwa ya wananchi kujiletea maendeleo. Kuanzia Morogoro hadi Rukwa, Mwanza hadi Ruvuma na Zanzibar, kote niliona kazi inaendelea. Serikali inatekeleza majukumu yake, wananchi wanajituma na mabadiliko yanaonekana.

Leo nitagusia baadhi ya masuala makubwa yaliyojiri mwaka tunaomaliza, changamoto tulizokabiliana nazo na tunayoyatarajia mwakani 2025.

Ndugu zangu;

Kama nilivyotangulia kusema kuwa mwaka 2024 ulikuwa ni wa kihistoria. Tuliadhimisha miaka 60 ya kuasiwa kwa Muungano wetu. Kama alivyowahi kusema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere "Tanzania ni nchi ya kuundwa na sisi wenyewe, kwa hiari yetu wenyewe, baada ya kukomboa sehemu zake kutoka katika Ukoloni." Hivyo basi, tuendeleo kujivunia na kuudumisha Utaifa wetu, uliojengwa katika misingi imara ya Muungano wa Jamii mbili zenye udugu wa asili.

Pamoja na kuadhimisha miaka 60 ya Muungano, tuliadhimisha pia miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, miaka 60 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, miaka 60 ya Jeshi la Polisi, na miaka 60 ya Mbio za Mwenge wa Uhuru.

Ni fahari kwamba tulifanya maadhimisho hayo yote huku nchi yetu ikiwa salama yenye Amani na Utulivu. Kwa hakika, ninavipongeza vyombo vya ulinzi na usalama

kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda nchi yetu. Nawashukuru pia wananchi kwa kuendelea kudumisha amani na umoja wa kitaifa; umoja ambao unaifanya Tanzania kuwa na sifa ya kipekee.

Ndugu Wananchi;

Mwaka huu pia tulikuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika kwa amani na utulivu. Katika uchaguzi ule, kwa mara ya kwanza, wagombea ambao hawakuwa na washindani ilibidi wapate ridhaa ya wananchi, kwa kupigiwa kura ya ndiyo au hapana. Hii imeondosha rasmi utaratibu wa kupita bila kupingwa, ambayo ni hatua kubwa katika ujenzi wa demokrasia nchini.

Ndugu Wananchi;

Mwaka 2024 ulikuwa wenye neema na mafanikio, hatuna budi kumshukuru Mungu kwa yote. Uchumi wa nchi yetu uliendelea kuimarika na kuwanufaisha wananchi. Kati ya Januari hadi Juni 2024 uchumi ulikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Deni la Taifa nalo liliendelea kuwa himilivu. Mfumuko wa bei umebaki ndani ya lengo la asilimia 3, hali iliyochangia na sera madhubuti za kifiedha.

Tulishuhudia ongezeko la uwekezaji kutoka ndani na nje ya Nchi. Kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kati ya Januari hadi Novemba 2024, tumesajili miradi ya uwekezaji 865 yenye thamani ya Dola za kimarekani bilioni 7.7 inayotarajia kuzalisha ajira 205,000.

Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), imetoa vibali vya kuwekezwa nchini viwanda vipya vikubwa 15 vyenye thamani ya Dola za Marekani milioni 235, vinavyotarajia kuzalisha ajira karibu 6,000 na kuuza nje bidhaa zenye thamani ya Dola za kimarekani milioni 94 kwa mwaka.

Kwa upande wa mapato, Mamlaka ya ukusanyaji Mapato Tanzania (TRA) imefanikiwa kukusanya Shilingi trilioni 21.276 kati ya mwezi Januari na Oktoba, 2024 sawa na asilimia 99.3 ya lengo. Hili ni ongezeko la asilimia 17.5 ikilinganishwa na makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Mwaka huu pia tumeendelea na jitihada za kujenga uchumi wa kidijitali kupitia matumizi ya TEHAMA. Katika kufanikisha hilo, tumeunda Wizara mahsusi ya TEHAMA na tayari tumezindua Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali. Miongoni mwa mipango yetu ya baadaye katika kutekeleza mkakati huo ni kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anatambulika kwa kutumia Jamii Namba, itakayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA).

Ndugu Wananchi,

SALAMU ZA MWAKA MPYA ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, KWA WATANZANIA, TAREHE 31 DISEMBA, 2024

Kwa upande wa Diplomasia, mwaka huu nchi yetu ilizidi kuimarika na kutuletea manufaa makubwa katika nyanja za kimataifa. Tumeepata heshima ya kushiriki Mkutano wa G20, ambao pamoja na maamuzi mengine yaliyofanyika, mkutano huo pia uliazimia kuunga mkono jitihada za upatikanaji wa nishati safi, na vile vile, uliazimia kuimarisha uwekezaji kwenye kilimo ili kuondosha njaa na umaskini duniani; jitihada zinazoendana na malengo yetu Tanzania.

Kwa mara nyingine tena, Tanzania iling'ara kwenye medani za kimataifa baada ya mgombea wetu Mheshimiwa Daktari Faustine Ndugulile kuwania na kushinda nafasi ya kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika. Hata hivyo, kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, Mheshimiwa Ndugulile alitua cha kabla hata ya kuingia ofisini. Tunazidi kumuomba pumziko la Amani.

Ndugu Wananchi,

Ziara tulizozifanya katika nchi 16 duniani, zilituwezesha kujenga mahusiano ya kidiplomasia, na kiuchumi. Ziara yangu nchini Jamhuri ya Korea, ilifanikisha kupatikana fedha zenye masharti nafuu kiasi cha Dola za kimarekani bilioni 2.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi katika sekta za maendeleo. Kupitia fedha hizo, pamoja na mambo mengine, tutajenga kituo cha kisasa cha mafunzo ya reli, chuo cha mafunzo ya anga na urubani, ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme Nyakanazi, na kituo cha uchenjuaji wa madini na maabara za kisasa za vito.

Miradi mingine itakayoangaliwa ni mradi wa Uendelezaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Ujenzi wa Kongani ya Viwanda Bagamoyo, na Ununuzi wa Mabeheva ya Abiria na Mizigo kwa ajili ya Kipande cha Reli kutoka Mwanza hadi Isaka, Ujenzi wa Bandari ya Wete na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo. Fedha hizo pia zitatumika kwenye Ujenzi wa Barabara Zanzibar, ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano Zanzibar, na Ujenzi wa Studio ya Filamu ya Kisasa na Kituo cha burudani mbalimbali kwa ajili ya ajira za vijana.

Ziara hiyo pia ilifanikisha kusainiwa kwa Mkataba wa masharti nafuu wenye kiasi cha Dola za Marekani milioni 163.6 kwa ajili ya kugharamia mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni na Kituo cha Mafunzo ya Afya huko Zanzibar.

Ziara ya nchini China, pamoja na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, ilifungua milango ya soko la bidhaa mbalimbali ikiwemo mihogo mikavu, soya, mabondo ya samaki, mazao ya baharini, asali, mashudu ya alizeti na pilipili. Ni matarajio yangu kuwa wakulima na sekta binafsi watachangamkia fursa hizi ili tuweze kunufaika na soko hilo. Wakati wa ziara hiyo, Tanzania, China na Zambia zilikubaliana kuifufua reli ya TAZARA ili kuboresha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo.

Kwa upande wa ukanda wa SADC tulipata heshima ya kupokea Uenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, yenye jukumu la kusimamia masuala ya Ulinzi na Usalama katika Kanda hiyo, ambapo mbali na masuala mengine tumeweza kusimamia uangelizi wa chaguzi kwenye Nchi za Botswana, Mauritius, Msumbiji na Namibia.

Ndugu Wananchi,

Kuimarika kwa uchumi kumetuwezesha kuendelea kufanya mabadiliko chanya katika mifumo yetu wa Elimu Msingi na Sekondari hadi vyuo vya ufundi. Tumeendelea kusogeza huduma bora za afya karibu zaidi na wananchi, kutandaza zaidi miundombinu ya umeme, na kusambaza umeme vijijini. Aidha, tumetekeleza dhamira ya kumtua mama ndoo kichwani, kwa kusimamia utekelezaji wa miradi 1,300 ya maji nchi nzima. Kukamilika kwa miradi hio kutatufikisha kutimiza lengo la asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini.

Katika sekta ya kilimo tulifanikiwa kuhamasisha kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kuboresha mifumo ya masoko ya mazao mbalimbali, na kupata bei nzuri ya mazao kwa wakulima. Kwa mfano, kwa mwaka 2024 ufuta uliuzwa kwa Shilingi 4,850 kwa kilo ikilinganishwa na Shilingi 3,600 mwaka uliopita 2023; Kahawa aina ya Arabika iliuzwa kwa Shilingi 8,500 kwa kilo ikilinganishwa na Shilingi 6,500 mwaka uliopita na kwa kahawa aina ya Robusta iliuzwa kwa Shilingi 5,000 kwa kilo badala ya shilingi 3,500 mwaka 2023. Mbaazi iliuzwa kwa Shilingi 2,236 kwa kilo mwaka 2024 badala ya Shilingi 2,000 mwaka 2023, kakao imeuzwa kwa Shilingi 35,000 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya Shilingi 29,500 mwaka uliopita 2023; na korosho iliuzwa kwa Shilingi 4,195 mwaka 2024 ikilinganishwa na Shilingi 2,190 mwaka 2023, huku uzalishaji wa korosho unatarajiwa kufikia tani 425,205 kwa msimu wa 2024/2025 unaoendelea ikilinganishwa na tani 310,787 zilizoalishwa msimu uliopita wa 2023/2024.

Mwelekeo wa Serikali ni kuboresha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kupitia soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa mazao ya kilimo.

Ndugu Wananchi,

Tukiangazia miradi ya kimkakati, baadhi yake tayari imefikia hatua ya kuanza kutoa huduma. Bwala la Mwalimu Nyerere limeanza kuzalisha umeme, na kufanya hali ya huduma za umeme nchini kuimarika. Uzalishaji kwa sasa umefikia jumla ya Megawatt 3,169 ikilinganishwa na mahitaji ya Megawatt 1,888.

Aidha, Mradi wa Reli ya Kisasa - SGR, unatoa huduma kutoka Dar es Salaam kupitia Morogoro hadi Dodoma. Shirika la Reli lilikuwa linasafirisha wastani wa abiria laki 3 hadi 4 kwa mwaka. Inafurahisha kwamba ndani ya miezi mitano ya huduma za SGR, zaidi ya abiria 1,200,000 wameshasafiri na reli hiyo.

Tumeendelea na maboresho kwenye sekta ya anga na uwekezaji kwenye shirika la ndege Tanzania. Mwaka huu, Shirika letu limefikisha ndege 16, na limeongeza safari za ndani ya nchi na kimataifa kufikia 25, ikiwemo kuanza tena safari za abiria kwenda Afrika Kusini na kukamilisha taratibu za kuanza safari za mizigo kwenda China. Mwaka huu Shirika limefanikiwa kusafirisha abiria zaidi ya milioni 1 na laki 1 na zaidi ya tani 10,000 za mizigo.

Serikali pia imeendelea kuwekeza kwenye miundombinu ya anga na kuboresha mifumo kwenye viwanja vya ndege. Mwaka huu tuliendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Arusha, Kahama, Mpanda, na Songwe. Mwakani tunatarajia kukamilisha viwanja vya ndege vya Iringa, Mtwara, Songea, Kigoma, Msalato, Musoma, Shinyanga na Sumbawanga.

Hapa nataka nisisitize kuwa, miradi hii ni yetu sote, na imejengwa kwa kutumia rasilimali zetu. Hivyo, tunawajibika kuitunza ili itunufaishe sisi na vizazi vijavyo kesho. Vitendo vya kuhujumu miradi hii ni kulihujumu Taifa.

Ndugu Wananchi,

Katika hatua nyingine, tuliendelea mageuzi ndani ya Serikali ili kuimarisha utendaji na ufanisi. Tuliendelea na zoezi la kubaini taasisi na mashirika yanayopaswa kufutwa, kuunganishwa au kurekebishwa kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi zaidi.

Mwaka huu pia tuliendelea kuchukua hatua za kuimarisha sekta ya ushirika ili kuchechea maendeleo vijijini. Dhamira ya Serikali ni kurejesha hadhi ya ushirika nchini. Ili kupata maendeleo endelevu kwa ushirika na wana-ushirika, Serikali imechagiza mchakato wa kuanzisha Benki ya Ushirika, ambayo iko katika hatua za mwisho, ikiwemo kufikia lengo la ukwasi wa shilingi bilioni 50.

Mwaka huu tuliendelea kushirikisha sekta binafsi na kuhamasisha uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) ili kuongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji na huduma. Katika kufanikisha hilo mpaka sasa kuna jumla ya miradi 74 ya Ubia ambayo ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi na utekelezaji. Hadi kufikia mwezi Desemba 2024, miradi 4 imefikia hatua ya utekelezaji, ambapo miradi miwili 2 ni ya uendeshaji wa bandari inayosimamiwa na TPA. Miradi mingine ni Ujenzi wa Jengo la Biashara (Business Complex) kubwa kuliko zote Kariakoo na ule wa Ubungo - East African Logistic.

Miradi mingine inayotazamiwa kuanza utekelezaji mwakani 2025 ni ujenzi wa barabara ya Haraka (Express way) kutoka Kibaha- Chalinze - km 78.9, mradi wa Ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto chini ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, mradi wa mabasi yaendayo kwa haraka (BRT) chini ya DART na mradi wa Ujenzi wa Jengo la Biashara na Hoteli ya Nyota Nne katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Ndugu Wananchi,

Katika kukabiliana na athari za mazingira kutokana na matumizi ya kuni, mwaka huu tulizindua Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia. Niwatake wahusika wasimamie ipasavyo utekelezaji wa Mkakati wa kuchechea matumizi ya nishati safi ili kufikia lengo la asilimia 80 ifikapo mwaka 2034. Aidha, nitoe rai kwa sekta binafsi kuchangamkia fursa zitokanazo na kukua kwa matumizi ya nishati safi.

Ndugu Wananchi;

Pamoja na kuwa ni mwaka wa kihistoria na mafanikio, mwaka 2024 pia ulikuwa na changamoto zake. Nitagusia zile kubwa na namna tulivyokabiliana nazo.

Changamoto moja kubwa tuliyokabiliana nayo ilikuwa ni athari za mvua za El Nino na Kimbunga Hiday, iliyosababisha mafuriko, maporomoko na upotevu wa maisha, uharibifu wa makazi, mashamba na baadhi ya miundombinu ikiwemo barabara na madaraja sehemu mbali mbali nchini. Tulisimama pamoja kama Taifa, misaada ya kibinadamu kwa waathirika kama vile vifaa vya ujenzi, chakula, nguo na malazi ilitolewa. Aidha, Serikali ilijenga nyumba 109 kwa ajili ya walioathirika na maporomoko kule Manyara.

Kupitia TANROADS na TARURA, Serikali ilitumia shilingi bilioni 136 kutengeneza miundombinu iliyoathiriwa. Pia tulitenga shilingi bilioni 868 kutekeleza miradi 70 ya kujenga miundombinu katika maeneo mbalimbali yaliyoathiriwa. Ni wazi kuwa, nguvu kubwa iliyotumika kushughulikia changamoto hiyo ya dhurura iliathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi ya barabara iliyokuwa inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Changamoto nyingine kubwa tuliyokabiliana nayo mwaka huu ilikuwa ni uhaba wa fedha za kigeni, hususan Dola ya Marekani. Hali hii iliathiri shughuli nyingi za biashara na uzalishaji. Katika kukabiliana na athari hizo, tuliunda kikosi kazi cha wataalam kilichotafiti hali hio na kushauri hatua za kuchukuliwa. Ushauri ulitongoza kutengeneza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni. Nafarikiwa kwamba, kufuatia utekelezaji wa Mkakati huo, upatikanaji wa fedha za kigeni umeimarika. Aidha, katika kuchukua hatua za kuhami uchumi wetu, Serikali imefanya uamuzi wa kuweka akiba ya taifa ya dhahabu katika Benki Kuu ya Tanzania, ili kuongeza uhimilivu wa uchumi wetu.

Katika mwaka 2024, nchi yetu ilikumbwa na jinamizi la ajali za barabarani. Takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania zinaonesha kuwa kati ya Januari hadi Disemba mwaka huu, nchi yetu ilishuhudia jumla ya ajali 1,735. Na ajali 1,198 kati ya hizo

SALAMU ZA MWAKA MPYA ZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, KWA WATANZANIA, TAREHE 31 DISEMBA, 2024

zilisababisha vifo vya ndugu zetu 1,715. Hii ni idadi kubwa sana. Ndugu zetu wengine 2,719 walijeruhiwa katika ajali za barabarani. Asilimia 97 ya ajali hizi zimetokana na makosa ya kibinadamu, kubwa kabisa ikiwa uzembe wa madereva, uendeshaji hatari na mwendo kasi ambayo kwa pamoja ni asilimia 73.7% ya ajali zote. Niwatake Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi Tanzania kungeza mikakati ya kuzuia ajali zinazosababishwa na makosa ya uzembe.

Ndugu zangu,

Katika kutatua changamoto hizo nilizoziainisha, tumedhihirisha uwezo wetu Kitaifa wa kukabili changamoto zinazojitokeza. Ninawashukuru sana wananchi wote kwa ustahimilivu, ushirikiano na uelewa wenu tunapopatwa na changamoto za aina hio. Hakika, tunauaga mwaka huu, tukiwa na faraja zaidi kwamba hakuna changamoto tuliyoshindwa kuikabili tunaposimama pamoja kama Taifa.

Ndugu Wananchi;

Kama mliyvosikia, pamoja na changamoto tulizokabiliana nazo, mwaka tunaomaliza, umekuwa wa mafanikio mengi yanayoimarisha ustawi wa wananchi. Katika mwaka tunaouanza muda mchache ujao, Serikali yetu itaendelea kuimarisha na kusambaza huduma za kijamii (Afya, Elimu, Maji na Umeme), tutachochea maendeleo kupitia ujenzi wa miundombinu, kuwaongezea fursa vijana na wanawake katika Biashara ndogo na za kati, na kuimarisha ustahimilivu wa Taifa.

Tutaendelea kukamilisha miradi ya kimkakati, ikiwemo Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, Daraja la Kigongo/Busisi ambalo limefikia asilimia 94, linalotazamiwa kukamilisha mwezi Februari, 2025. Tutatoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa kama vile Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma na kurahisisha usafiri na usafirishaji katika miji inayokuwa kwa kasi.

Miongoni mwa miradi hii ni mradi wa Barabara za Mzunguko katika Jiji la Dodoma ambao umefikia asilimia 80, upanuzi wa Barabara ya Uyole-Ifisi-Songwe Airport jijini Mbeya ambao umefikia asilimia 20, na Awamu ya Tatu na Nne ya miundombinu ya barabara za mwendo kasi jijini Dar es Salaam, huku tukianza huduma kwenye Awamu ya Pili kwa njia ya Mbagala iliyokwishakamilika.

Mapema mwakani, tunatazamia Reli ya SGR, ianze kusafirisha mizigo kwa vipande vya Dar es Salaam hadi Dodoma kiasi cha tani milioni 1 kwa mwaka, lengo ni kukuza ushoroba wa kibiashara na kimaendeleo unaochochea uzalishaji na ajira kwa wananchi kote inapopita. Vile vile, tutakamilisha kipande cha Mwanza hadi Isaka na kukifanya kianze kutoa huduma. Ujenzi wa vipande vyengine hadi Kigoma vitaendelea kujengwa kama ilivyopangwa.

Ndugu Wananchi,

Katika juhudi za kuvutia Michezo na Mikutano ya Kimataifa, Serikali itajenga viwanja na maeneo yenye sifa za Kimataifa kwa ajili hiyo. Mbali na ukarabati mkubwa unaofanywa katika viwanja vya mpira wa miguu vilivyopo, nchi yetu inaendelea kujenga viwanja vyengine kule Arusha na Dodoma. Kama mnayofahamu mwezi Februari 2025, nchi yetu inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya CHAN na mwaka 2027 kutachezwa mashindano ya AFCON. Sambamba na miundombinu ya michezo tumeanza jitihada za kujenga na kurekebisha kumbi za mikutano katika viwango vya kimataifa ili tuweze kuvuta mikutano mingi zaidi. Kwa kuwa nchi yetu imebeba ajenda ya upatikanaji wa nishati safi Afrika, tumepata heshima ya kuwa wenyeji wa Mkutano kuhusu masuala ya nishati kwa Bara la Afrika (Africa Energy Summit) unaoandaliwa kwa ushirikiano wa Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika utakaofanyika mwezi Januari 2025.

Ndugu Wananchi,

Nchi yetu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Falsafa ya R4, inayohimiza Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga nchi yetu. Vile vile, tunaendelea uhuru wa habari unaoashiriwa na idadi kubwa ya vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza, na uhuru kutoa maoni kupitia vyombo mbalimbali; na hata uhuru wa kukusanyika na kujumuika.

Tutaendelea mchakato wa kupata maoni ya Wananchi ili tukamilishe uandishi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 mapema mwakani ili tuanze utekelezaji wake. Niwapongeze wananchi wote waliochangia katika mchakato huu, na niwasihie tuendele kutoa maoni yetu hadi mchakato utakapokamilika.

Katika hatua nyingine, mwakani tutapokea Ripoti ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi ambayo itatusaidia kuboresha wigo na mifumo ya kodi, pamoja na kustawisha mazingira ya kibiashara nchini.

Katika utekelezaji wa mapendezo ya Tume ya Haki Jinai, mwakani 2025 tutakamilisha Sera na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusiana na masuala ya haki jinai. Tutaendelea pia kutoa msaada wa kisheria kwa wahitaji. Hadi sasa, jumla ya wananchi 495,552 wameshanufaika na Msaada wa Kisheria wa Kampeni ya Mama Samia Legal Aid chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Ndugu zangu;

Mwaka 2025 ni mwaka maalum kwa maendeleo ya kisiasa na kidemokrasia nchini. Tutafanya Uchaguzi Mkuu kuwachagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Madiwani, na kwa upande wa Zanzibar, tutachagua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na

Madiwani. Miongoni mwa maandalizi ya awali ya uchaguzi huo, ilikuwa ni kufanya mashauriano na wadau wote wa kisiasa yaliyopelekea kurekebishwa kwa sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, na Sheria ya Vyama vya Siasa. Ni imani yetu kwamba sheria hizo zitatuongoza vyema katika kusimamia kwa ufanisi chaguzi zijazo. Nitoe rai kwa wananchi na wadau wote wa uchaguzi kuhakikisha tunaidumisha sifa ya Nchi yetu ya kuwa na demokrasia iliyojengeka juu ya msingi wa uhuru na haki.

Ndugu Wananchi;

Nilianza kwa kusema kuwa mwaka tunaomaliza ulikuwa mwaka wa kihistoria, wenye mafanikio na unaotupa matumaini zaidi kuhusu kesho ya Taifa letu; na maelezo yangu yameonesha kwa nini nilisema hivyo. Nikihitimisha, niseme tu kwamba, mwenendo mzuri wa uchumi, uwezo wa kukabiliana na changamoto na kusimamia mipango yetu, na ari kubwa ya wananchi kujitelea maendeleo, vinatupa sote matumaini makubwa sana tunapoingia mwaka 2025. Nimalizie kwa kuwashukuru sana kwa imani na ushirikiano mkubwa mliotoa kwa Serikali na kutuwezesha kutekeleza vyema majukumu yetu. Nitoe shime kwa Watanzania kujenga ari na ujasiri wa kufanya kazi kwa uadilifu, weledi, bidii na maarifa zaidi, katika kuchangia maendeleo yetu.

Katika mwaka ujao 2025 na mengine mingi ijayo, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie afya njema na furaha mioyoni mwetu. Tujaaliwe uwepo wa Amani na Utulivu nchini, kheri na fanaka katika maisha yetu.

**Mungu ibariki Afrika,
Mungu ibariki Tanzania,
Ahsanteni kwa kunisikiliza!**

**Nawatakiwa mwaka mpya wenye kheri.
Asante.**






MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu